# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA

**26 MEI, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA – 26 MEI, 2016

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

## II. MASWALI YA KAWAIDA:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**239. MHESHIMIWA MOSHI SELEMANI KAKOSO (MPANDA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Wilaya ya Mpanda ndiyo pekee inayotoa huduma za Kimkoa katika Mkoa wa Katavi kwa kutumia bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda:-

Je, ni lini Hospitali ya Mkoa itajengwa**.**

**240. HUSSEIN MOHAMMED BASHE (NZEGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wakati wa kampeni za uchaguzi Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa daraja la Nhobola na daraja la Butandula pamoja na barabara inayounganisha Kijiji hicho na Kijiji cha Mbogwe:-

Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa ahadi ya ujenzi wa madaraja hayo pamoja na barabara zake.

**241. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa/Vijiji wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu sana hali wakiwa ndio viungo wa shughuli za maendeleo katika jamii:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza kuwalipa mshahara au posho Wenyeviti wa Mitaa au Vijiji;

(b) Je, kwa nini Madiwani wasiwe na ofisi zao kama ambavyo Wabunge hupewa ofisi zao;

(c) Je, ni lini ofisi za Wenyeviti wa Mitaa au Vijiji zitajengwa ili kuepusha kuwa na ofisi majumbani kwao.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

### 242. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa ardhi kati ya Hifadhi ya Mpanga na wananchi wa Wilaya ya Wanging'ombe.

## WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

### 243. SIXTUS RAPHAEL MAPUNDA (MBINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Kumekuwa na ongezeko la Kampuni kubwa kuanzisha mashamba ya Kahawa katika maeneo ya Wilaya ya Mbinga na sehemu za Songea Vijijini jambo linalotishia uzalishaji na soko kwa Wakulima wadogo wadogo wa Kahawa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalinda wakulima wadogo wasimezwe na wakulima wakubwa.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

**244. MHESHIMIWA DANIEL NICODEMUS NSANZUGWANKO (KASULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Mkoa wa Kigoma ni kati ya Mikoa mitatu inayopata mvua nyingi katika nchi yetu kwa wastani wa takribani milimita 1300 kwa Mwaka ikifuatiwa na Mkoa wa Katavi:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali haifanyi jitihada ya kuwekeza katika kilimo ili kunufaika na uwepo mzuri wa hali ya hewa;

(b) Je, ni kwa nini Mkoa wa Kigoma uliondolewa katika Mikoa yenye uzalishaji mkubwa na kupata mgao mdogo wa pembejeo;

(c) Je, ni kwa nini Kituo cha Mbegu cha Bigoga kilichopo Wilaya ya Kasulu kimetelekezwa.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**245. MHESHIMIWA RIZIKI SHAHARI MNGWALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Serikali ilijenga Gati kubwa la Kilindoni katika Wilaya ya Mafia kwa mabilioni ya fedha ili kuwezesha meli kubwa kutia nanga na hivyo kutatua tatizo sugu la usafiri wa majini Wilayani Mafia, lakini licha ya

Gati hilo kukamilika na kuzinduliwa rasmi na Rais aliyepita Mhe. Jakaya Kikwete tangu Mwaka 2013, bado Gati hilo halijaanza kutumika jambo ambalo limesababisha wananchi kuendelea kupata adha kubwa ya usafiri kwa kutumia bahari:-

Je, ni lini Serikali itaelekeza Meli kubwa na Boti zenye viwango na bima kuanza kuwahudumia wananchi wa Mafia kwa kutumia Gati la Kilindoni.

**246. MHESHIMIWA ELIAS JOHN KWANDIKWA (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kata za Uyogo, Igwamanoni, Ushetu na Chena katika Jimbo la Ushetu hazina mawasiliano ya simu za mkononi ya uhakika:-

Je, ni lini maeneo hayo yatapatiwa mawasiliano ya simu za mkononi yenye uhakika.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

### 247. MHESHIMIWA TAUHIDA CASSIAN GALLOSS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka uzio kwenye vituo vikubwa vya polisi vilivyopo Zanzibar.

## WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

### 248. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Serikali kupitia Mfumo wa Bima ya Taifa ilitoa tenda kwa Kampuni moja binafsi kwa ajili ya kufunga mfumo wa kielektroniki wa kutunza kumbukumbu za wagonjwa na taarifa za Bima:-

(a) Je, ni fedha kiasi gani ilitumika kwa hospitali hizo kufungiwa mfumo huo;

(b) Je, ni kwa kiasi gani Serikali ilizingatia thamani halisi ya fedha (*value for money*) ukilinganisha na mahitaji makubwa katika sekta ya afya kama madawa, vifaa tiba na watumishi.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**DODOMA**
**26 MEI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA